


# MAHUSIANO YETU TANO (5) NA MUNGU:

## UHUSIANO WETU WA NNE; "MTOTO/MWANA NA BABA(KE)" - "WANA WA MUNGU"

Hujambo!

Nakusalimu asubuhi ya leo.

**UTANGULIZI:**
Tumekuwa tukijadili mahusiano yetu matano na Mungu:
- Sisi ni viumbe wake (Chapisho la 11).
- Tunachagua kutii chini ya upendo wa Mungu kama watumwa chini ya Bwana wao (Chapisho la 12).
- Tunatembea na Yesu (Mungu) kama marafiki (Chapisho la 13).

Sasa tunasonga mbele kwa uhusiano wetu wa nne na Mungu: uhusiano wa Mungu na wanawe (watoto wake), yaani BABA na Mtoto, ama BABA na MWANAWE.

**MUNGU BABA ANATHIBITISHA YESU KUWA MWANAWE WA PEKEE:**
Yesu anaiongoza njia kama Mwana wa pekee wa Mungu. (Maelezo zaidi kuhusu uhusiano wa Yesu na Baba yatakuwa katika chapisho lijalo.)

Mungu anamthibitisha Yesu kuwa Mwana wake wakati wa ubatizo wake:

> **LUKA 3:21** *Ikawa, watu wote walipokwisha kubatizwa, na Yesu naye amebatizwa, naye anaomba, mbingu zilifunuka*; **22** *Roho Mtakatifu akashuka juu yake kwa mfano wa kiwiliwili, kama hua; sauti ikatoka mbinguni; "Wewe ndiwe Mwanangu, mpendwa wangu; nimependezwa nawe*".

Mungu anamthibitisha Yesu kuwa Mwana wakati wa kugeuka kwa sura yake:

> **LUKA 9:35** *Sauti ikatoka katika lile wingu, ikisema, Huyu ni Mwanangu, niliyemchagua; msikilizeni*

Mungu anamthibitisha Yesu kama Mwana katika Wiki ya Mateso:

> **YOHANA 12:28** *Baba, ulitukuze jina lako. Basi ikaja sauti kutoka mbinguni, Nimelitukuza, nami nitalitukuza tena*.

**MUNGU AMEKUSUDIA KUTUFANYA KUWA WANA WAKE**:
Mpango wa kustaajabisha wa Mungu ni kutubadilisha sisi, ambao sote ni viumbe walioanguka na wenye dhambi kuwa, wana wake wa kiasili.

> **WARUMI 8:29** *Maana wale aliowajua tangu asili, aliwachagua tangu asili wafananishwe na mfano wa Mwana wake, ili yeye awe mzaliwa wa kwanza miongoni mwa ndugu wengi*.

> **WARUMI 9:8** *yaani, si watoto wa mwili walio watoto wa Mungu, bali watoto wa ile ahadi wanahesabiwa kuwa wazao*.

> **YOHANA 1:12** *Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio jina lake*; **13** *waliozaliwa, si kwa damu, wala si kwa mapenzi ya mwili, wala si kwa mapenzi ya mtu, bali kwa Mungu*.

**KWA WALIO WANAWAKE**:
Kwa wasomaji wetu wanawake ambao wanaweza kuhisi kubaguliwa na Agano Jipya linalozungumza kuhusu “wana (wa kiume) wa Mungu,” elewa kwamba umejumuishwa kama “wana”.

Katika ulimwengu wa zamani (kama katika tamaduni zingine leo) watoto wa kiume walithaminiwa zaidi kuliko wa kike.

Lakini chini ya Agano Jipya, msimamo wa wanawake umeinuliwa sana. Wajibu hutofautiana kwa wanaume na wanawake, lakini msimamo wa kiroho mbele za Mungu, wote ni sawa. Kwa hivyo wanaume na wanawake kwa pamoja wanaitwa "watoto wa Mungu".

**WAGALATIA 3:26** *Kwa kuwa ninyi nyote mmekuwa wana wa Mungu kwa njia ya imani katika Kristo Yesu*. **27** *Maana ninyi nyote mliobatizwa katika Kristo mmemvaa Kristo*. **28** *Hapana Myahudi wala Myunani. Hapana mtumwa wala huru. Hapana mtu mume wala mtu mke. Maana ninyi nyote mmekuwa mmoja katika Kristo Yesu*. **29** *Na kama ninyi ni wa Kristo, basi, mmekuwa uzao wa Ibrahimu, na warithi sawasawa na ahadi.*

(KUMBUKA: Kwa upande mwingine, sisi wanaume tumejumuishwa katika Bibi-arusi wa Kristo!)

**BAADHI YA VIPENGELE VYA KUWA WANA (WATOTO) WA MUNGU**:

1. Sisi ni utimilifu wa unabii wa Agano la Kale

   **2 WAKORINTHO 6:18** *Nitakuwa Baba kwenu, Nanyi mtakuwa kwangu wanangu wa kiume na wa kike, asema Bwana Mwenyezi*.

2. Tunapendwa sana na baba yetu wa mbinguni

   **1 YOHANA 3:1** *Tazameni, ni pendo la namna gani alilotupa Baba, kwamba tuitwe wana wa Mungu; na ndivyo tulivyo. Kwa sababu hii ulimwengu haututambui, kwa kuwa haukumtambua yeye*.

3. Yesu anatuunganisha kuwa Watu wamoja (*ona pia Waefeso 2:11-22*)

   **YOHANA 11:51-52** *Na neno hilo yeye hakulisema kwa nafsi yake; bali kwa kuwa alikuwa Kuhani Mkuu mwaka ule, alitabiri ya kwamba Yesu atakufa kwa ajili ya taifa hilo*. **52** *Wala si kwa ajili ya taifa hilo tu; lakini pamoja na hayo awakusanye watoto wa Mungu waliotawanyika, ili wawe wamoja*.

4. Sisi ni wazao wa kweli wa Ibrahimu

   **WAGALATIA 3:7** *Fahamuni basi, ya kuwa wale walio wa imani, hao ndio wana wa Ibrahimu*.

5. Sisi ni wapokeaji wa Roho wake Mtakatifu

   **LUKA 11:13** *Basi, ikiwa ninyi mlio waovu mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vyema, je! Baba aliye mbinguni hatazidi sana kuwapa Roho Mtakatifu hao wamwombao*?

   **WAGALATIA 4:6** *Na kwa kuwa ninyi mmekuwa wana, Mungu alimtuma Roho wa Mwanawe mwetu, aliaye, Aba, yaani, Baba*.

   **WARUMI 8:14** *Kwa kuwa wote wanaoongozwa na Roho wa Mungu, hao ndio wana wa Mungu*. **15** *Kwa kuwa hamkupokea tena roho wa utumwa iletayo hofu; bali mlipokea roho ya kufanywa wana, ambayo kwa hiyo twalia, Aba, yaani, Baba*. **16** *Roho mwenyewe hushuhudia pamoja na roho zetu, ya kuwa sisi tu watoto wa Mungu*;

6. Katika Yesu tunapata uwezo wa kumfikia Baba daima

**WAEFESO 2:18** *Kwa maana kwa yeye sisi sote tumepata njia ya kumkaribia Baba katika Roho mmoja*.

7. Sisi ni warithi pamoja na Kristo Yesu

**WAGALATIA 4:6** *Na kwa kuwa ninyi mmekuwa wana, Mungu alimtuma Roho wa Mwanawe mioyoni mwetu, aliaye, Aba, yaani, Baba*. **7** *Kama ni hivyo, wewe si mtumwa tena bali u mwana; na kama u mwana, basi, u mrithi kwa Mungu*.

**WARUMI 8:17** *na kama tu watoto, basi, tu warithi; warithi wa Mungu, warithio pamoja na Kristo; naam, tukiteswa pamoja naye ili tupate na kutukuzwa pamoja naye*.

8. Sisi ni watoto wa Nuru

**YOHANA 12:36** *Maadamu mnayo nuru, iaminini nuru hiyo, ili mpate kuwa wana wa nuru. Hayo aliyasema Yesu, akaenda zake, akajificha wasimwone*.

**WAEFESO 5:8** *Kwa maana zamani ninyi mlikuwa giza, bali sasa mmekuwa nuru katika Bwana; enendeni kama watoto wa nuru*, **9** *kwa kuwa tunda la nuru ni katika wema wote na haki na kweli*; **10** *mkihakiki ni nini impendezayo Bwana*.

9. Tunachagua kuishi maisha matakatifu, ya haki, na yenye upendo

> **WAFILIPI 2:14** *Yatendeni mambo yote pasipo manung'uniko wala mashindano*, [15] *mpate kuwa wana wa Mungu wasio na lawama, wala udanganyifu, wasio na ila kati ya kizazi chenye ukaidi, kilichopotoka; ambao kati ya hao mnaonekana kuwa kama mianga katika ulimwengu*, [16] *mkishika neno la uzima; nipate sababu ya kuona fahari katika siku ya Kristo, ya kuwa sikupiga mbio bure wala sikujitaabisha bure*.
>
> **1 YOHANA 3:10** *Katika hili watoto wa Mungu ni dhahiri, na watoto wa Ibilisi nao. Mtu ye yote asiyetenda haki hatokani na Mungu, wala yeye asiyempenda ndugu yake*.

10. Sisi ni wapenda amani

> **MATHAYO 5:44** *lakini mimi nawaambia, Wapendeni adui zenu, waombeeni wanaowaudhi*, [45] *ili mpate kuwa wana wa Baba yenu aliye mbinguni; maana yeye huwaangazia jua lake waovu na wema, huwanyeshea mvua wenye haki na wasio haki.*

11. Tunatiwa adabu na Mungu kama watoto wake

> **WAEBRANIA 12:5** *tena mmeyasahau yale maonyo, yasemayo nanyi kama kusema na wana, Mwanangu, usiyadharau marudia ya Bwana, Wala usizimie moyo ukikemewa naye*; [6] *Maana yeye ambaye Bwana ampenda, humrudi, Naye humpiga kila mwana amkubaliye*.

12. Yesu atakaporudi tutabadilishwa kuwa kama yeye

> **WARUMI 8:23** *Wala si hivyo tu; ila na sisi wenyewe tulio na malimbuko ya Roho, sisi pia tunaugua katika nafsi zetu, tukikutazamia kufanywa wana, yaani, ukombozi wa mwili wetu*.
>
> **1 YOHANA 3:2** *Wapenzi, sasa tu wana wa Mungu, wala haijadhihirika bado tutakavyokuwa; lakini twajua ya kuwa atakapodhihirishwa, tutafanana naye; kwa maana tutamwona kama alivyo*.

13. Marafiki huja na kuondoka - Wana hudumu milele

> **ZABURI 23:6** *Hakika wema na fadhili zitanifuata Siku zote za maisha yangu; Nami nitakaa nyumbani mwa BWANA milele*.

SWALI: Je, unajua kwa hakika wewe ni mwana wa Mungu?

WIKI IJAYO: ***UHUSIANO WETU WA 5 NA MUNGU***!

Ubarikiwe sana katika jina la Yesu.

Ni wako

Douglas

Douglas Van Devender.
Huduma za 'Jesus Ministries International' na 'Transforming Prayer'.